

Bibilia ya watoto  
Inaleta

Yesu awachagua  
wasaidizi kumi na  
wawili



Kimeandikwa na: Edward Hughes

Kimeorodheshwa na: Byron Unger; Lazarus

Imerekebishwa na: E. Frischbutter; Sarah S.

Kimetafsiriwa na: Grace Chepkoech

Kimedhibitishwa na: Bible for Children  
[www.M1914.org](http://www.M1914.org)

©2013 Bible for Children, Inc.

License: Kuna ruhusa ya kuchapa hadithi hii,  
lakini bila ya kuuza.



Yesu alitenda mambo ya ajabu.  
Aliponya magonjwa, ...



... aliwapa watu wenye shida amani moyoni na akilini mwao na alifunza neno la Mungu.



Halaiki ya watu ilimjia Yesu kwa  
usaidizi na uponyaji.



Akaamua kuchagua watu kumi na wawili kutokana na wale waliokuwa wakimfuata, ...



... ili wamsaidie katika  
kazi ya Mungu.



Kama una amuzi  
la kufanya, je  
wewe umwomba  
Mungu? Yesu  
alifanya hivyo!





Katika mlima  
mnyamavu  
alizungumza na  
Baba yake wa  
mbinguni. Yesu  
aliomba hadi  
jua ilipotua.





Yesu  
aliomba usiku  
mzima pia.

Asubuhi, Yesu akawaita  
wote waliokuwa wakimfuata -  
marafiki wote waliokuwa  
wakimhudumia na kumtii.



Kutokana nao akawachagua  
kumi na wawili wasaidizi wa  
kipekee au mitume.




Wawili wa kwanza kuchaguliwa walikuwa mandugu, Simioni Petro na Andrea. Waliwacha biashara yao ya kufua samaki Yesu



alipowaita  
iliwamfuate.



Yakobo na Yohana,  
wana wa Zebedayo,  
pia walicha biashara yao ya  
kufua samaki.



Yesu pia aliwachagua Filipi,  
Batholomeo, Mathayo,  
Thomasi, Simioni wa  
Ziloti, Yakobo  
mwana wa  
Alfayo, ...



... Yuda ndugu ya Yakobo  
na Yuda Iskariote  
ambaye mwishowe  
alimsaliti  
Yesu.






Yesu alifunza kuwa kutii  
aliyoyasema ilikuwa  
kama kujenga  
nyumba juu ya  
mwamba.




Mvua ikinyesha  
na mafuriko  
yakija nyumba  
ile haitaanguka.



Lakini wasiotii neno lake ni kama  
kujenga nyumba juu ya mchanga.  
Mvua ikinyesha na mafuriko yakija  
nyumba ile itaanguka.



Amri zingine za Yesu hazikuwa rahisi. "Mtu akikupiga ushavuni wa kulia, mpe pia wa kushoto aupige," Alifunza.



"Mpende adui wako."  
Watu wanaitaji usidizi  
wa Mungu kuishi  
kama Yesu.



Yesu aliwaambia watu waombe  
kwa siri - wasijionyeshe katika  
maombi mbele ya watu  
kama wafarisayo  
wengine.



Yesu alisema  
Mungu angewalisha  
na kuwavisha watu  
waliomwamini.



Jinsi Mungu aliwapa  
ndege chakula na  
kupea maua rangi  
za kupendeza, ...






... angewapa  
waliomwamini  
walichohitaji.



Yesu aliwafunza wasaidizi wake aliowachagua vitu vingi siku hiyo. Alipomaliza, mtu mwenye ukoma akaja na kumwomba Yesu amponye.




Yesu akamjibu, "Nitakuponya. Kuwa mzima sasa." Watu walipokuwa wakitazama mtu yule mwenye ukoma akawa safi. Alikuwa amepona!



Mwana wa Mungu peke ndiye  
angeweza kutenda yale.

Wasaidizi wake  
walijua kuwa  
walikuwa na  
mwalimu wa  
ajabu.



Yesu awachagua wasaidizi kumi na wawili

Hadithi kutoka kwa Neno la Mungu,  
Bibilia,

inapatikana katika

Mathayo 4-7, Marko 1, Luka 6

"Kufafanusha maneno yako kwatia nuru."

Zaburi 119:130



Mwisho



Hii hadithi ya bibilia inatueleza kumhusu  
Mungu wetu wa ajabu aliyetuumba na  
anayetaka tumjue.

Mungu anajua tumetenda mambo mabaya,  
anayoyaita dhambi. Adhabu ya dhambi ni  
mauti, lakini Mungu anakupenda sana hata  
akamtuma mwana wake wa pekee, Yesu, Ili  
afe msalabani na aadhibiwe kwa dhambi  
yako. Alafu Yesu akafufuka na kuenda  
nyumbani mbinguni! Ukimwamini Yesu na  
kumwomba msamaha kwa dhambi yako,  
Atakusamehe! Yesu atkuja na kuishi ndani  
yako, na utaishi naye milele.



Kama unaamini huu ni ukweli, Sema haya  
kwa Mungu:

Mpendwa Yesu, ninaamini kuwa wewe ni  
Mungu, na ulifanyika mtu ili ufe kwa ajili ya  
dhambi zangu, ili niwe na maisha mapya, na  
siku moja nitaenda kuwa nawe millele.  
Nisaidie nikutii na niishi kwa ajili yako kama  
mtoto wako. Amina.

Soma bibilia na uzungumze na Mungu kila  
siku! Yohana 3:16

